**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

Namba za simu
Mkuu wa Shule : 0714297725
Makamu Mkuu wa Shule :0685156481/0689260930
Barua pepe:nakapanyasecondaryschool@yahoo.com

Shule ya Sekondari NAKAPANYA
S.L. P 333
**TUNDURU – RUVUMA**

Kumb.Na. NKSS/SS/1/02

Kwa

…………………………………………………………………

**YAH: TAARIFA YA KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NAKAPANYA ……………………………….**

Nafurahi kukutarifu kuwa Umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii kwa mwaka……………… katika tahasusi ya **"……."**. Nakupongeza na kukukaribisha hapa shuleni, nina imani utafurahia na kunufaika na mambo yanayoendeshwa hapa shuleni. Nategemea kwamba muda wote utashirikiana na wanafunzi wenzako, walimu na wafanyakazi wengine katika kutoa mchango wako wa mawazo na vitendo ili kuleta na kudumisha sifa nzuri ya shule hii.

Shule hii ipo umbali wa Kilometa sitini na nne (64) mashariki mwa mji wa Tunduru barabara ya kuelekea DAR ES SALAAM. Usafiri wa basi kutoka Tunduru mjini unapatikana katika kituo cha Mabasi Tunduru, nauli ni shilingi 5,000/= hadi NAKAPANYA. Kwa wanafunzi watakaoanzia safari Dar es Salaam wanapaswa kupanda gari ziendazo SONGEA kwa njia ya LINDI na watashukia kituo cha NAKAPANYA, (Magari kampuni ya MANNING NICE, BARAKA CLASSIC, SUPERFEO NA NEWFORCE.) Watakaotokea mikoa mingine wanapaswa kufika SONGEA mjini na watapanda gari za kwenda MASASI AU MTWARA AU DAR ES SALAAM na watashukia kituo cha NAKAPANYA.

Pamoja na barua hii naambatanisha fomu zifuatazo;

a) Fomu ya kujiunga na shule (Joining instructions)
b) Fomu ya taarifa ya mwanafunzi. (Ijazwe na mzazi na kuileta shuleni na kukabidhi siku ya kuripoti)
c) Fomu ya uchunguzi wa afya.

Mwisho nakufahamisha kuwa Muhula wa masomo unaanza tarehe ………………….. Hivyo, mwanafunzi unapaswa kuwasili shuleni tarehe ……………………… ukiwa umevaa sare ya shule. Mara ufikapo shuleni utapokelewa na mwalimu wa zamu na atakupeleka ofisi ya Makamu wa Mkuu wa Shule kwa usajili.

Karibu NAKAPANYA Sekondari.

DONATUS LAWRENCE NYANDOA
MKUU WA SHULE

**SHULE YA SEKONDARI NAKAPANYA**

**FOMU YA MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE (JOINING INSTRUCTION).**

## 1.0. Mambo Muhimu ya kuzingatia.

### 1.1. Sare ya shule.

i) Sare ya shule hii ni mashati mawili (02) meupe mikono mirefu na suruali mbili (02) za kitambaa cha suti rangi ya dark bluu (**Dark blue**) yenye urefu na upana unaozingatia urefu wa mwili wako. Kumbuka, suruali isiwe ya mshono wa jeans au modo.Tai mbili ndefu rangi ya bluu (**dark blue**) sawiana suruali ya shule.

ii) Viatu vyeusi vya kufunga na Kamba vyenye visigino vifupi na vifunike miguu.

iii) Sweta moja rangi ya **KIJIVU** (GREY), soksi rangi nyeusi ndefu na isiwe na urembo.

iv) Mkanda wa rangi nyeusi, uwe wa ngozi usiwe na madoa na urembo wowote.

v) Ufike na Vesti za kutosha na nguo nyingine za ndani za kutosha.

- Sare ya michezo ni bukta na fulana (Jezi) rangi ya **NJANO** (**Jezi ya taifa stars**), Raba na soksi ambazo zitavaliwa viwanjani wakati wa michezo tu. Pia traki suti rangi ya**KIJIVU** moja itavaliwa muda wa maandalizi ya jioni (Preparation).

vi) Mwanafunzi afike naFulanayenye rangi ya **UGORO** (yenye kola shingoni), aidha kwa wale watakaohitaji itapatikana shuleni kwa bei ya shilingi elfu kumi na mbili tu (12,000/=).

vii) Nguo za kushindia (Shamba dress) ni;

- Suruali zakutosha rangi KIJIVU kitambaa cha suti mshono sawa na suruali ya shule na Fulana mbili (form six) za rangi**UGORO**. Nguo nyingine zilizo nje ya maelekezo hazitakubaliwa ni vyema ukaziacha nyumbani.
- Mtindo wa ushonaji wa sare ya shule kwa muda wa masomo umeambatanishwa katika fomu hii (Rejea picha ya mwanafunzi iliyopo ukurasa wa mwisho)

### 1.2. Michango mbalimbali.

**Michango ya lazima inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni;**

| Na | Aina ya mchango | Kidato V | Kidato VI |
|---|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= | |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= | |
| 3. | Nembo | 5,000/= | |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= | |
| | **JUMLA KUU** | **80,000/=** | |

- Fedha hizo zilipwe kwenye **akaunti ya shule namba**, **70901100063, NAKAPANYA Sekondari, katika Benki ya NMB.** (Tafadhali andika jina la mwanafunzi na siyo jina la mzazi au mlezi na kidato katika karatasi yako ya malipo - Pay in Slip).
- Shule haitoi huduma ya chakula maalumu (Special diet) kwa wanafunzi wenye matatizo ya afya.

### 1.3. Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni;

i) Picha (passport size) mbili (2).

ii) Ream mbili A4 (2) ya karatasi kwa mwaka (Ikabiziwe siku ya kuripoti shuleni).

iii) Daftari za masomo zisizopungua saba (Counter books Quire 3).

iv) Peni, rula na kalamu za kutosha.

v) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (Orodha imeambatanishwa).

vi) Scientific calculator moja, Mkebe (Kwa wanafunzi wa Geography).

vii) Godoro (futi 2.5) kwa wanafunzi wa bweni.

viii) Mashuka pair mbili (2) rangi ya kijani kibichi (Light green), blanketi 01, foronya 01 na chandarua 01.

ix) Vyombo vya chakula (Sahani, bakuli, kijiko na kikombe).

x) Kila mwanafunzi afike na Sabuni ya maji (Ujazo wa Lita 5).

xi) Vifaa vya usafi viletwe kwa mgawanyo ufuatao.

| Na. | Aina ya tahasusi | Aina ya kifaa cha usafi anachostahili kuleta |
|---|---|---|
| 1. | HGK | Jembe moja (01) ,mopa (01) na ndoo (01) litre 10,mfagio laini wa ndani |
| 2. | CBG | Jembe moja(01),mopa (01),ndoo (01),mfagio laini wa ndani |

## 2.0. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

## 2.1. Sheria na Kanuni za Shule

i) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.

iii) Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation).

iv) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.

v) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

vi) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

vii) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

viii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

ix) Kutunza mali za shule.
x) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari.
xi) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

## MUHIMU.

i) Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.
ii) Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.
iii) Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

### 2.2. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i) Wizi
ii) Kutohudhuria masomo kwa Zaidi ya siku 90 bila taarifa au utoro.
iii) Kugoma au kuhamasisha mgomo.
iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake , walimu au walezi na jamii kwa ujumla.
v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
vi) Kufuga ndevu.
vii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
viii) Uvutaji sigara na matumizi ya dawa za kulevya.
ix) Uasherati , uhusiano wa jinsi moja, kuoa na kuolewa.
x) Kupata ujauzito au kuolewa.
xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii) Kusababisha mimba au kumpa mimba mwanafunzi.
xiii) Kuhudhuria kumbi za starehe na nyumba za kulala wageni.
xiv) Kumiliki, kukutwa au kumiliki simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xv) Kudharau bendera ya taifa.
xvi) Kufanya jaribio lolote la kujiua, kuua au kutishia kujiua kamakunywa sumu.
xvii) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**KIAMBATANISHO 1. NKSS.K5.C**

**SHULE YA SEKONDARI NAKAPANYA**

**ORODHA YA VITABU**

**A. HISTORY**

1. TIE (2016) History for Secondary Schools: Form Five - Tanzania Institute of Education

2. TIE (2016) History for Secondary Schools: Form Six - Tanzania Institute of Education
3. Tumaini , S.C.K (2010). Contemporary Historical Events: Advanced Level History One. Dar es Salaam: Shgibitali & Sons publishers.
4. Yassin S ( ). Essentials in Advanced Levels History Paper 2, Dar es Salaaam.

**GEOGRAPHY**

1. A Comprehensive Approach to Physical Geography – D.T Msabila.
2. Elementary Physical Geography: Advanced Level and Colleges – Ahmed Lubwana.
3. Practical Geography. Map reading, Photographs, Research and Surveying – Zisti Kamili.
4. Geography for Secondary Schools: Form Five – Tanzania Institute of Education (2016).

## B. KISWAHILI

### a) KISWAHILI 1

1. Nadharia ya Lugha ya Kiswahili: Kidato cha tano na sita – Nyambari Nyangwine na Masebo (2010).
2. Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo – Kihore, Y.m na Masamba, D.P.B: TUKI (2003).
3. Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la Pili: English – Swahili Dictionary – TUKI.

### b) FASIHI.

1. Nadharia ya Fasihi kidato cha Tano na Sita – Masebo – Oxford University Press.
2. Tahakiki Vitabu Teule vya Fasihi Kidato cha Tano na Sita - Nyangwine na Masebo.

**TAMTHILIA**

1. Kivuli kinaishi – Saidi Ahmed Mohamed – Oxford University Press.
2. Kwenye Ukingo wa Thimu – Ibrahim Hussein – Oxford University Press
3. Nguzo Mama – Penina Muhando (1982)
4. Morani – Emmanuel Mbogo (1993).

**RIWAYA**

1. Vuta Nkuvute – 4th edition - Mbunda Msokile (2009)
2. Kufikirika 4th ed – Shaban Robert – Mkuki na Nyota
3. Mfadhili – Hussein Tuwa (2007) – Macmillan Aidan
4. Usiku Utakapokwisha – 2nd ed - Mbunda Msokile (2007) – Macmillan Aidan

**USHAIRI**

1. Kimbunga : Toleo la Tatu – Haji Gora Haji (1995) TUKI.
2. Chungu Tamu – Theobald Mvungi.
3. Mapenzi Bora – Shaban Robert – Mkuki na Nyota Publishers.
4. Fungate ya Uhuuru - Mohamed S. Khatibu – Macmillan Aidan

**GENERLA STUDIES**

1. Nyangwine , C.M , Bukagire C.R & Maluka S.O (2010) . Contemporary Approach for Advanced Level: General Studies Notes form 5 & 6.
2. Bigirwamungu , J & Deogratius S.M (2012). Understanding Advanced Level General Studies: Advanced Level Secondary Schools.

**CHEMISTRY**

1. Tie (2025) General chemistry for advanced level secondary school, students book, Dar es salaam.
2. Tie (2025) Physical chemistry for advanced level secondary school, student book 5 and 6, Dar es salaam.

3. Tie (2025) Organic chemistry for advanced level, secondary school, student Book 6 Dar es salaam.
4. Tie (2025) Inorganic chemistry for advanced level secondary school student book 6, Dar es salaam.

**BIOLOGY**

1. Tie (2025) Biology for advanced secondary school, student book 5, Dar es salaam.
2. Tie (2025) Biology for advanced secondary school, student book 6, Dar es salaam.

**KIAMBATANISHO 1. NKSS.K5. A**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU SHULE YA SEKONDARI NAKAPANYA**

**FOMU YA TAARIFA ZA MWANAFUNZI MATSS.K5.**

1. Jina kamili la mwanafunzi:……………………………………………………………………
2. Kidato ulichojiunga hapa shuleni………………………………Mchepuo:………………
3. Jina la mzazi/mlezi:…………………………………………………………………………

   Anuani yake…………………………………………Kazi yake………………………………

   Simu za mkononi 1:……………………………………2:…………………………………

   3:……………………………………4:…………………………………

4. Mahali ulipozaliwa (Mwanafunzi).

   (i) Mkoa…………………………… Wilaya ………………… Kata……………

   (ii) Tarafa…………………………… Kijiji cha …………………………………

   (iii) Tarehe ya kuzaliwa ………………………………………………

5. Mahali unapoishi sasa………………………………………………………………………

   Anuani yako………………………… Namba za simu……………………………………

6. Dini/dhehebu lako……………………………………………………………………………
7. Unaishi na Baba tu/mama tu/wazazi wote/mlezi……………………………
8. a) Jina la shule ya msingi ulikosoma……………………………………………………

   b) Jina la shule za sekondari ulizosoma…………………………………………………

   - Shule ya sekondari uliyoanzia…………………………Anuani………………………
   - Shule ya sekondari uliyomalizia………………………Anuani……………………

**MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO/FUJO NA MAKOSA YA JINAI.**

Mimi…………………………………(mwanafunzi),naahidi kuwa sitajihusisha/sitashiriki katika kupanga,kufanya wala kushabikia migomo,fujo au ghasia zozote au makosa ya jinai nikiwa **Nakapanya**Sekondari katika muda wangu wa uanafunzi.

Saini ya mwanafunzi:…………………………………………………………………………

Majina ya Mzazi/Mlezi:………………………………………………………………………

Saini ya Mzazi/Mlezi:……………………………………………Tarehe:……………………………






**<u>KIAMBATANISHO 2.  NKSS.K5.B</u>**

**HALMASHAURI YA WILAYA TUNDURU**

**SHULE YA SEKONDARI NAKAPANYA**

**S.L.P P.O BOX 333, TUNDURU – RUVUMA.**

**Barua pepe: nakapanyasecondaryschool@yahoo.com**

(Request for Medical Examination)

This form is to be completed by a Medical Officer.

Name of student:………………………………………………… Age: …….. Sex: …………

The above named has been examined in respect of:

a) STOOL ……………………………………………………………………………

b) URINE……………………………………………………………………………

c) CHEST ……………………………………………………………………………

d) BLOOD …………………………………………………………………………

e) EYES ……………………………………………………………………………

f) EARS ……………………………………………………………………………

g) HEART …………………………………………………………………………

h) STOMACH ULCERS ………………………………………………………………

i) OTHERS

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

I am satisfied / not satisfied that the above named Student is physically and mentally /not physically and mentally fit to pursue further studies in Secondary School.

…………………………………    ……………………

SIGNATURE(and official stamp)DATE

………………………

DESIGNATION    ………………….

STATION